JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**

Telegram **"AFYA", DODOMA**
Nambari ya Simu: **+255 026 – 2323267**
Baruapepe: ps@afya.go.tz

Mji wa Serikali Mtumba,
Barabara ya Afya,
S. L. P 743,
**40478 DODOMA.**

## TAARIFA KWA UMMA NA VYOMBO VYA HABARI

## MAADHIMISHO YA WIKI YA FAMASI

**Dodoma, Jumatano Juni 16, 2021.**

Leo ni kilele cha wiki ya Famasi iliyoanza tarehe 10 Juni 2021. Wiki ya Famasi ilianzishwa ili kutambua mchango wa wataalam wa Kada ya Famasi katika kuwahudumia wagonjwa. Wiki ya Famasi ni njia muhimu ya kuwakumbusha wanataaluma wa kada ya Famasi popote walipo kutimiza wajibu wao wa kuwahudumia wagonjwa kwa kuzingatia miiko na maadili ya kitaaluma ili kuimarisha afya za Watanzania. Aidha, ni wiki muhimu kwa Jamii kutambua mchango wa Wafamasia katika kuwahudumia wananchi. Ujumbe wa mwaka huu unasema ***"Timu madhubuti: Kufanya kazi kwa pamoja na Wafamasia kuboresha huduma kwa wagonjwa"***.

Hivyo, tunapoadhimisha wiki hii, ni vyema kutafakari na kuyakubali majukumu yetu kwa ujumla. Niwakumbushe kuwa upatikanaji wa dawa ni jukumu lenu la msingi na sio ajenda ya bajeti peke yake bali ni usimamiizi sehemu ya kazi. Aidha, ni jukumu la msingi kusimamia menejimenti ya dawa kwenye mnyororo wote wa ugavi na usambazaji ili zisipotee au kuibiwa na wale wachache wenye nia mbaya kwa taifa. Vilevile, ni muhimu kusimamia matumizi sahihi ya dawa ikiwa ni pamoja na wanataaluma kutoa elimu kwa wagonjwa na kuwapa taarifa sahihi ili kupata matokeo mazuri ya matibabu.

Mwisho, nizikumbushe na kuziomba kamati za ulinzi na usalama kuwa dawa ni moja ya ajenda muhimu inayogusa uhai wa binadamu, hivyo, ni vema zikashiliki kikamilifu katika kuhakikisha zinalindwa na kutumika ipasavyo ili kuokoa maisha ya Wananchi. Usimamizi shirikishi wa bidhaa za afya ukijumuisha viongozi wa vijiji, mitaa, kata, halmashauri na mikoa

ni muhimu sana katika kuhakikisha dawa na bidhaa nyingine za afya zinakuwa salama na zinawafikia wananchi. Kwa uelewa huu Wizara inaelekeza yafuatayo:

1. Makatibu Tawala Mikoa, Wakurugenzi wa Halmashauri kwa pamoja na Waganga Wakuu wa Mikoa na Halmashauri kuzifufua kamati shirikishi za huduma za afya kuanzia ngazi ya vijiji, mitaa, kata, halmashauri na mikoa ili kusimamia na kukagua mara kwa mara huduma za dawa na vifaa tiba katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini;
2. Wafamasia wazingatie uwajibikaji na uadirifu katika kuhakikisha upatikanaji wa dawa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya nchini; na
3. Wataalamu wote kuzingatia matumizi sahihi ya miongozo na nyenzo nyingine mbalimbali katika utoaji wa huduma na usimamizi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi vya maabara.

***"Tufanye kazi kwa pamoja na Wafamasia kuboresha huduma kwa wagonjwa"***

Imetolewa na

Prof. Abel N. Makubi
**KATIBU MKUU (AFYA)**